

## Matumizi ya Intaneti Kandarasi kwa Wanafunzi na Walezi

### Mwanafunzi

Nimesoma “Sera ya Matumizi ya Intaneti Yanayokubalika” ya Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence. Naelewa na kukubali kufuatilia masharti ya ombi hili la kufikia mtandao, na sheria za Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence kwa matumizi yanayokubalika ya rasilimali za mtandao.

Naelewa ya kwamba nawajibika kibinafsi kwa gharama zote na ada, ikijumuisha ununuzi wa simu nje, uchapishaji na ununuzi wa bidhaa unaofanywa kupitia mtandao. Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence haihusiki na miamala kama hiyo na haitawajibika kwa gharama au uharibifu wowote, iwe wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, unaotokana na miamala ya mtandao na mtumiaji.

Zaidi na hayo, nakiri ya kwamba mtandao wa kompyuta wa a Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence inamilikiwa kipekee na Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence na ya kwamba faili zozote, rekodi, barua ya kieletroniki au mawasiliano mengine inaweza kukaguliwa, kuhariri, au kufutwa na Wilaya ya Shule ya Providence wakati wowote, kulingana na sera au sheria za Wilaya ya Shule ye Umma ya Providence. Kwa kawaida, barua ya kielektroniki katika akaunti binafsi hazita kaguliwa bila idhini ya mtumaji au mpokeaji, isipokuwa kama inahitajika kuchunguza malalamiko.

Naelewa pia ya kwamba ikiwa nitakiuka, upendeleo wa ufikiaji wangu unaweza kusitishwa, na nidhamu ya shule na/au kitendo cha sheria kinaweza kuchukuliwa dhidi yangu. Kwa kuzingatia matumizi ya muunganisho wa mtandao wa Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence na kuwa na ufikiaji katika mitandao ya umma, Kwa wakati huu naondoa Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence na washiriki wake wa Bodi ya Shule, wafanyakazi na wakala kutoka kwa madai yeyote na uharibifu unao tokea kutoka kwa matumizi yangu, au kutoweza kutumia mtandao.

Naelewa ya kwamba matumizi ya Intaneti ni upendeleo, sio haki. Naelewa zaidi ya kwamba ukiukaji wowote wa miongozo hapa juu itasababisha usitishaji mara moja wa upendeleo wangu wa Intaneti, na kwa sababu ya ukiukaji huo hatua zingine za nidhamu zinaweza kuchukuliwa.

---

Chapisha Jina la Mwanafunzi

---

Sahihi ya Mwanafunzi

---

Tarehe ya Sahihi

**MZAZI/MLEZI**

Mimi ndiye mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliye tajwa hapo juu. Nimesoma “Sera ya Matumizi Yanayokubalika ya Intaneti” ya Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence. Naelewa na kubaliana na vipengele, sheria na masharti yaliyo angaziwa ndani yake. Kwa sasa napatia mtoto wangu ruhusa ya kutumia huduma ya intaneti inayo tolewa na Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence. Naelewa ya kwamba mtoto wangu ana hitajika kufuatilia sera hii. Naelewa zaidi ya kwamba kuna uwezekano wa mtoto wangu kufikia taarifa kwenye intaneti ambayo haifai kwa wanafunzi na ya kwamba bidii inayowezezana itafanywa kwa upande wa shule na wafanyakazi wa Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence kuzuia ufikiaji wa taarifa kama hiyo, lakini mtoto wangu ako na wajibu mkuu wa kujizuia mwenyewe dhidi ya hii taarifa isiyofaa.

---

Chapisha Jina la Mzazi/Mlezi

---

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

---

Tarehe ya Sahihi